

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI**

**SHULE YA SEKONDARI PAGWI**

**S. L. P. 71**

**SIMU NA - 0734100340/0699247701**

**Kumb. Na. PSS/S.30/3/vol. 6**

**JINALA MWANAFUNZI:.....**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI PAGWI KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.**

**1. UTANGULIZI;**

Ninafurahi kukuharifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kati ya Shule ya Sekondari Pagwi kwa mwaka 2021. Shule ipo katika Kijiji cha Lumotio Kata ya Pagwi kwa umbali wa KM 55 kutoka Songe (Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi) Kusini.

Muhula wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**, hivyo anatakiwa kuripoti Shule kuanzia tarehe **2/01/2021**, ndani siku saba (7) kushindwa kuripoti kwa muda uliopangwa unaweza kupoteza nafasi ya masomo hapa Shuleni.

Shule hii ya kutwa (Day School) Hivyo mwanao atalala nyumbani na kuja Shuleni kila siku na kurudi nyumbani baada ya shughuli za shule kuisha.

Shule inaandaa utaratibu wa kuwa na Hosteli kwa watoto wa kike kwa wale wanaokaa vijiji vya mbali, utaratibu utakapo kamilika utafahamishwa

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA;**

**SARE ZA SHULE**

**A. WAVULANA**

Suruali mbili (2) rangi ya damu ya mzee na shati mbili nyeupe mikono mifupi, Sweta samu ya mzee na viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba visiwe na visigino virefu wala shungo ndefu. Suruali kawaida ikiwa na mifuko mitatu (3) marinda mawili kulia na mawili kushoto na ruksi sita (6), mkanda wa kuvalia uwe mweusi na upana usizidi nchi 1<sup>1/2</sup>.

**B. WASICHANA**

Sketi mbili (2) rangi ya damu ya mzee na shati nyeupe mikono mifupi, sweta rangi ya damu ya mzee, soksi nyeupe na viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba, visiwe na visigino virefu wala shingo ndefu. Sketi iwe rinda biksi ndefu ya kuvuka magoti, vazi la hijabu ni sheti ndefu na nusu kanzu vizingatie rangi ya shule.

**ANGALIZO;** Sketi fupi na suruali ya kubana (Modo) ndala na makubazi (Sandalasi) haziruhusiwi shuleni. Mwanafunzi atakaye vaa kinyume na maelekezo hapo juu ataondolewa shuleni

**3. 0. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHA KUKUSIMAMISHA AU KUFUKUZA SHULE.**

Ni marufuku kabisa mwanafunzi kujihusisha na;

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Kupiga au kupigana
- e) Kuona au kuolewa
- f) Kusababisha au kupata mimba
- g) Kutoa mimba
- h) Kudharau wimbo au bendera ya Taifa
- i) Kuharibi kwa makusudi mali ya uma
- j) Kuwa na simu ya mkononi (Akija nayo atanyang'anywa na haito rudishwa)
- k) Kukataa adhabu kwa makusudi
- l) Kugoma, kuchochea, kuongoza au kushiriki mgomo au vulugu, amani ya shule au watu
- m) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile, Bangi, Mirungi, Kubeli, Cocaine nk.
- n) Kutembea baa, vilabu vya pombe, majumba ya sherehe na majumba ya kufikia wageni

**4. 0. VIFAA**

Kila mwanafunzi alete vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi na shughuli mbalimbali za kilimo, panga, fyekeo, jembe, ufagio na ndoo moja ya lita 10

**5. 0. MAMBO YANAYOPASWA KUZINGATIWA NA KILA MWANAFUNZI**

- i. Kila mwanafunzi ni lazima kukamilisha na kuwasilisha Shuleni fomu zifuatazo;
  - a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali
  - b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusi historia ya mwanafunzi, na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
  - c) Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na Shule.
- ii. Kila Mwanafunzi lazima ahudhurie vipindi vyote vya masomo na vya nje ya darasa na kushiriki kikamilifu. Ni kosa kupiga kelele darasani au katika mikutano au mikusanyiko mingine
- iii. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na School Bag kwa ajili ya kubebea vifaa vya Shule. Kila mwanafunzi anawajibika kutunza mali za shule na mali zake binafsi.

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamiligu.

**KARIBU SANA PAGWI SEKONDARI**

*Peter*  
...PETER GEDAM... NSUNUWE  
**MKUU WA SHULE**  
PAGWI SEKONDARI  
11/11/11